

SHULE YA UPILI YA MTAKATIFU CLARE
KAZI YA LIKIZO

- 1· Ni nini maana ya nyimbo zifuatazo. (al· 5)
- (i) Tenzi
 - (ii) bembelezi
 - (iii) Sifo
 - (iv) nyiso
 - (v) hodiya
 - (vi) mbolezi
- c) Eleza umuhimu wa nyimbo (al· 8)
- d) Eleza sifa za wimbo wa aina ya Bembelezi (al· 5)
- 2· (a) Eleza maana ya miviga kisha uonyeshe inakotumika (al· 7)
- (b) Eleza sifa za miviga (al· 5)
 - (c) Onyesha umuhimu wa miviga (al· 8)
- 3· (a) Eleza maana ya methali. (al2)
- (b) Eleza sifa za methali (al· 5)
 - (c) Onyesha umuhimu wa methali katika jamii (al· 8)
- 4· a Jadili sifa tatu zinazotambulisha shairi. (alam 6)
- b)(i) Eleza maana ya malumano ya utani katika fasihi simulizi. (alam 2)
- (ii) Kwa nini ni muhimu kujifunza fasihi simulizi. (alam 8)
- 5) (i) Vitendawili ni nini katika fasihi simulizi? (al· 2)
- (ii) Eleza sifa zozote nne za vitendawili (al· 2)
 - (b) Onyesha tofauti kati ya vikundi hivi: (al· 6)
 - (i) Hekaya na Hurafa
 - (ii) Visakale na Visasili - (iii) Ngano za mtanziko na Ngano za mazimwi

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali

Hapo zamani za kale, Murungu (Mungu) alimtuma kinyonga kwa watu. Alimwambia “Nenda kwa waja wangu na uwaeleze kuwa mtu akifa, awekwe nyuma ya nyumba na baada ya siku mbili atafufuka.”

Kinyonga akaanza safari. Alitembea polepole akapanda milima na kuvuka mabonde. Njiani akakutana na sungura. Sungura akamuuliza, “Unaenda wapi kinyonga?” Kinyonga akamjibu, “Naenda kwa watu kuwapelekea ujumbe kutoka kwa Mungu kuwa mtu akiaga dunia awekwe nyuma ya nyumba kwa muda wa siku mbili kisha ataweza kufufuka.”

Sungura hakufurahia jambo hilo. Akamwambia kinyonga kwa vile ana mbio, amwachie jukumu hilo apeleke ujumbe huo kwa watu. Kinyonga hakukubali. Hivyo sungura alimwacha kinyonga na kuchana mbuga.

Sungura alikimbia kukurukakara hadi kwa watu. Alipowasili alimwambia “Nimetumwa na Mungu,” Watu waliposikia hivyo, wakafungua masikio yao. “Nimeambiwa na Mungu kuwa mtu akifa, afe alale na kuzikwa mara moja.” Nusura watu wamuue kwa kuleta ujumbe huo. Wengine walitaka kumfanya kitoweo lakini sungura akatoroka.

Sungura akiwa njiani kurudi alimwona kinyonga kwa mbali. Akajificha kichakani. Sungura alisukuma jiwe kubwa akielekeza alikokuwa kinyonga. Jiwe lilimwangukia kinyonga pu! Na kumuua papo hapo.

Sungura alipofika kwa Mungu na kumweleza aliyowaambia watu, Mungu alikasirika ja mkizi. Alimvuta masikio yakawa marefu na kumwonya asiseme

uwongo tena. Kinyonga hakufikisha ujumbe. Watu waliamini ujumbe wa sungura. Mpaka sasa watu huamini ujumbe ulioletwa na sungura.

Maswali

- (a) (i) Hii ni hadithi ya aina gani? (alama 1)
(ii) Toa sababu. (alama 1)

- (b) Taja sifa zinazoitambulisha hadithi hii kama fasihi simulizi. (alama 3)
(c) Taja maudhui ya hadithi hii. (alama 3)
(d) Taja aina mbili za matumizi ya lugha kwenye hadithi. (alama 3)
(e) Hadithi hii ina umuhimu gani katika jamii. (alama 4)

sarufi

1·Huku ukitoa mifano fafanua njia tano za miundo ya silabi za kiswahili

(al 5)

2·Fafanua maana ya istilahi zifuatazo kisha utolee mifano:

- i) silabi
- ii)mofimu
- iii)kiambishi awali na kiambishi tamati
- iv)kihusishi
- v)vichangamano